# TORATI AMA NEEMA

Habari za jioni, marafiki. Naam, nina furaha kuwa huku tena usiku wa leo. Nami. . .sababu ya kuchelewa, nilininii tu. . .Naam, kama Ndugu Neville alivyosema, ni—nilikuwa ninachelewa. Lakini kilichosababisha hilo, nilikuwa. . .Hivi majuzi nilisema, kanisani, mnajua, nilisema, "Vema, nilikuwa ninaenda tu kujaribu kujiepusha na simu na kadhalika." Huwezi kufanya hivyo. Na kwa hiyo nimetoka tu hospitalini hivi punde, hospitali kadhaa huko Louisville, dakika chache tu zilizopita, dharura. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu nilichelewa kidogo tu. Nilifika tu kwa wakati mzuri kuja huku. Kwa hiyo, halafu mimi. . .mke wangu alikuwa, naamini, alinipigia simu na kuniambia habari zake. Ninaamini, Dada Ruddell angekuwa hapa usiku wa leo, naye alikuwa mgonjwa, pia. Na kwa hiyo hakika nachukia kusikia hivyo.

2 Nami nilimwacha binamu yangu huko Louisville, ndio kwanza nimwongoze kwa Kristo, jambo moja zuri. Na—na ulikuwa ni ugonjwa wa kutisha, ni kansa ya glandi za limfu, na angeweza kufa wakati wowote. Naamini Bwana alimponya, mara moja.

3 Kwa hiyo mjukuu wa Ndugu Jim Wiseheart amelala kule na kitu kile kile, Hospitali ya Askari Wastaafu, na kansa ya glandi za limfu imeenea karibu na moyo na mvungu wa kifua, kwa hiyo mnajua hiyo inamaanisha ana muda kidogo. Hakuna wanachoweza kufanya juu yake, lakini wanajua tumaini lao pekee ni Mungu.

4 Kweli napaswa kwenda Milltown, usiku wa leo. Busty Rogers, mnakumbuka, huja hapa. Wengi wenu ninyi watu mnamjua Ndugu Rogers. Yuko mahututi, wamenipigia simu, siku nzima.

5 Na maskini Georgie Carter kule chini, aligundua, aliponywa yapata miaka kumi na miwili, kumi na minne iliyopita, amelazwa kitandani muda wa miaka tisa na miezi minane, wala kamwe hakutoka kwenye kitanda hicho. Nami nikiwa huko nje wakati mmoja. . .Nilikuwa nimemwombea mara kadhaa. Basi nikatoka usiku mmoja, nami nilikuwa mahali fulani nikiomba. Ndipo Bwana akashuka, huku Nuru ndogo ikiangaza kwenye kichaka cha miti midogo, kasema, "Shika njia ya kwenda kwa Carter, kwa ajili ya uponyaji wa Georgie. Atapata afya." Ninyi nyote mnajua kisa hicho, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Miaka hii yote, hajapata angalau kulala kitandani, hata angalau kwa mafua, nadhani, tangu wakati huo.

6 Nasi tunaona ya kwamba yuafa, akiwa na kansa ya titi sasa. Naye amekuwa akipiga simu. Alisikia nimerudi. Walisema tayari alikuwa amekata tamaa. Aliamka akatoka kitandani kukubali uponyaji wake; kwa hiyo sina budi kumwona. Kesho ndiyo siku yangu ya mwisho hapa; sina budi kuondoka. Kwa hiyo, lundo la simu, karibu *hivyo*, hata hujui la kufanya. Inakubidi tu kufanya vizuri uwezavyo.

7 Lakini jambo kuu, kama ndugu alivyosema, jambo kuu la kufanya, inakubidi kuacha kila kitu kwa ajili ya ushirika wako na Yesu Kristo. Kila kitu! Maana, hata hivyo, tukianza kuangaliana mmoja na mwenzake, basi tunamwacha Kristo, mnaona. Afadhali nitumie muda mwingi tena mwingi sana nikishiriki Naye, upate kuwasaidia wengine. Hiyo ni kweli?

8 Kwa hivyo ni vema ku—kuwa humu usiku wa leo kwa ajili ya mkutano huu mdogo wa maombi, ambapo sisi hukusanyika hapa Jumatano usiku. Na nilikuwa nimesahau kumwambia kuhusu kufundisha usiku wa leo. Kwa hiyo, hapa, sina budi kuja hapa usiku wa leo na kufungua tu. Kwa hiyo, wakati nikishuka huku, kwa taa za gari langu, nilichagua kitu hapa ambacho nilikuwa nikifundisha Shule ya Jumapili, si muda mrefu uliopita, kwenye Kitabu cha Waebrania, kwa ajili ya usiku wa leo.

9 Ninaamini mara ya mwisho nilipokuwa nikifundisha shule ya Jumapili hapa, loo, kabla ya kwenda ng'ambo, nilikuwa katika Waebrania mlango wa 10. Nakumbuka nikiendelea kusoma, ndipo nikaweka alama hapa, kifungu cha 18, "kwa ajili ya Jumapili ijayo," nayo hiyo Jumapili ijayo haijawahi kufika bado. Kwa hiyo labda tutaanzia hapo, usiku wa leo, kwa ajili ya somo letu la jioni.

Bwana awabariki. Na muwakumbuke hawa wote katika maombi.

10 Mama mmoja ndio kwanza aniambie, muda mfupi uliopita, wakati nikiingia. Rafiki yangu wa kale, huko nje hospitalini, ama chini hospitalini, hasa, naye ndio kwanza afanyiwe upasuaji. Bill Grant kwenye kikosi cha polisi hapa, rafiki yangu mwema, huzichapisha hizo picha na kadhalika; hospitalini, kwa dharura.

11 Na—nami nikakutana na kaka ya Ndugu Slaughter kule nyuma. Gene aliniambia, naamini, alikuwa hospitalini mara mbili. Na ni magonjwa tu kila mahali, mwajua. Hakuna mwisho wake, karibu. Lakini alisema . . .

12 Mnajua, mara nyingi nimeshangaa, wakati Musa alipowaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani. Alipowatoa, kulikuwa na yapata watu milioni mbili. Hao ni vijana kwa wazee, wote pamoja. Naye aliwaongoza kwa muda wa miaka arobaini nyikani. Sasa hebu fikiria jinsi gani, sasa, huko nje bila—bila usafi ambao tungekuwa nao leo. Na wao, pia, hawakuwa na . . . Walikuwa na vijana, vijana wengi sana pale.

Unafikiri ni watoto wangapi walizaliwa usiku mmoja, na watu milioni mbili? Na halafu, pamoja na hayo, pamoja na wazee wote, na vilema na kadhalika. Naye aliwaongoza miaka arobaini, chini ya uongozi wa Mungu. Huko nyikani miaka arobaini, na, walipotoka, hapakuwa na hata mmoja aliye dhaifu miongoni mwao.

13 Hivi hamngependa kuangalia katika mkoba wa dawa wa Dk. Musa, usiku wa leo, kuona alichokuwa nacho mle ndani ili kuwadumisha—kuwadumisha wazima? Je, nyote mngependa kuuangalia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninaweza kuwaonyesha. Tutarudi hapa sasa katika Kutoka, nami nitaonyesha ni wapi. Hili ndilo kasha lake la dawa. Nitawaonyesha alichosema hapa nyuma. Nitaangalia moja kwa moja kwenye gunia lake la dawa, na nitaona linavyosema.

14 Wakati mtoto alikuwa azaliwe, wakati mtu aliposhikwa na kidole tumbo, au alipoambukizwa TB, ama chochote kama hicho, haya hapa maagizo ambayo Musa alisoma, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Hicho ndicho kitu pekee alichokuwa nacho. "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Sasa, hicho ndicho kitu pekee alichokuwa nacho. Uh-huh. Hicho ni kizuri vya kutosha, sivyo? Musa alisema, "Sasa, Bwana Ndiye aliyekuponya." Ndipo wakamwombea tu, naye akapona.

15 Na mnajua jambo lingine lililotukia wakati huo nyikani? Hata hawakuhitaji viatu vipya walipotoka, wala nguo zao hazikuchakaa. Miaka arobaini nyikani na dawa moja tu, agizo moja, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." Naye alifanya hivyo kwa sababu waliliamini Neno Lake, na kujiweka tu huru na kila . . .

16 Kumbukeni, sasa, walikuwa wamefundishwa. Walikuwa huko chini na Wamisri, ambao walikuwa werevu kuliko wote. Hatuna madaktari, siku hizi, wenye akili kama walivyokuwa. Kwa sababu, walikuwa na mambo waliyofanya, ambayo yanaonyesha ya kwamba hatujafika mahali hapo, bado, katika sayansi. Kwa mfano, Wamisri walijenga . . . Siku chache tu zilizopita, nilipita karibu na sfiniksi kule, ili kuangalia jinsi kitu hicho kilivyokuwa kikubwa.

17 Na hayo mapiramidi, mbona, kule juu, marefu kuliko bloku ya mji, hewani, kuna tani nyingi. Kuna majabali kule juu karibu makubwa kama maskani hii. Wasingeweza kuyanyanyua huko juu siku hizi hata wafanye nini. Kwa hivyo, walifanya hivyo kwa njia fulani.

18 Halafu basi, hiyo sfiniksi, nadhani inachukua mabehewa kumi na sita kuuwekelea mguu wake. Na mwili wake je? Nayo imekaa huko juu sana hewani. Waliipandishaje kule juu? Mnaona, walikuwa—walikuwa watu ambao walikuwa na siri, akili ambayo hatuna siku hizi. Nafikiri tunayo, lakini hatujaendelea mbele nayo, atomiki ama kitu kama hicho; kwa

sababu, nguvu za umeme, ama hakuna nguvu kama hizo, zingeweza kuiinua. Lakini waliijenga wakati huo.

19 Na hiyo piramidi, ile piramidi kubwa iliyo pale, kijiografia, ni kamilifu sana katikati ya dunia; haijalishi jua liko wapi, kamwe hakuna kivuli karibu nayo. Uhandisi, tuna ninii nyingi. . . tungali mbali sana, kujilinganisha nao. Pia, kuwazia, hiyo imekuwa ni zaidi ya miaka elfu tano iliyopita, walikuwa na hizo.

20 Kwa hiyo, mle ndani, wanaona Biblia, ni sawa tu na Biblia hii hapa, imeandikwa mle, kwa vipimo tu na kadhalika, hupima Injili na Maandiko, kama tu tulivyo Nayo hapa. Henoko aliiweka mle, miaka na miaka kabla ya kipindi kilichotangulia ile gharika.

21 Na, basi, Mungu aliandika Biblia tatu. Mungu hufanya kila kitu kwa tatutatu. Aliandika Biblia tatu. Alikuwa na kuja mara tatu kwa Kristo. Kuna vipindi vitatu vya neema. Kuna nafsi tatu katika Uungu. . . madhihirisho matatu ya Nafsi moja katika Uungu, hasa. Na mambo hayo yote. Mnaona?

22 Sasa, kama vile Yesu alivyokuja mara ya kwanza, amekuwa hapa mara moja (sivyo?), Yeye alikuja kumkomboa Bibi-arusi Wake. Anakuja mara ya pili kumpokea Bibi-arusi Wake, kumnyakua, kukutana hewani. Kisha anakuja mara ya tatu pamoja na Bibi-arusi Wake, kama Mfalme na Malkia.

23 Mnaona? Kwa hiyo, basi, kuna tatu pia, zile tatu katika madhihirisho ya Mungu. Mungu alijidhihirisha Mwenyewe mara moja katika Ubaba, alipokuwa akiwaongoza wana wa Israeli. Wakati mwingine Mungu alipojidhihirisha Mwenyewe ilikuwa katika Uwana, Bwana Yesu Kristo. Mara ya tatu Mungu alipojidhihirisha Mwenyewe, yuko pamoja nasi sasa, Roho Mtakatifu. Mnaona, madhihirisho matatu. Kila kitu katika tatutatu.

24 Sasa hebu tuingie katika somo letu. Ni wangapi wanaopenda kusoma Biblia, na kuninii tu. . .? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, ninaipenda sana.

25 Mungu akipenda, nitakaporudi. . . Nitaninii. . . naondoka nikapumzike kidogo sasa, kwa juma moja au mawili. Kwa hiyo, nitakaporudi, Mungu akipenda, ninataka kufanya uamsho hapa maskanini, wa uamsho wa mafundisho tu. Nasi tutachukua mahali fulani katika Biblia, na tupitie tu kwenye ninii yetu. . .

26 Kumbukeni, ni wazee wangapi hapa ndani wanakumbuka tulipokuwa tukichukua kama vile Kitabu cha Kutoka, na kukichukua labda kwa miezi na miezi, bila kuachana na Kutoka?

27 Niliingia kwenye Ayubu wakati mmoja, na ni kama sikukiacha. Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mwanamke mmoja akaniandikia barua, akasema, "Ndugu Branham, kweli utawahi kumwondoa Ayubu

kwenye lundo la majivu?" Niliendelea na somo hilo moja, maskini mzee Ayubu, akiketi pale nje kwenye lundo la majivu, mwajua. Marafiki zake wote walimwacha, alitokewa na majipu na kila kitu. Nilimhurumia sana maskini jamaa huyo, mpaka nikaninii. . .

28 Halafu, basi, jinsi Bwana alivyogeuka na kumbariki, kwa sababu aliishi vizuri sana alivyojua, chini ya sa—sadaka ya kuteketezwa. Hivyo ndivyo tu alivyojua, naye. . .kuungama dhambi zake. Naye akaenda na kuchukua watoto wa—wake, akatoa dhabihu, kasema, "Huenda wamefanya dhambi kisiri, wala hawajui." Jinsi alivyokuwa baba halisi, naye Mungu akamrudishia watoto hao wote, mwishowe. Mlijua hilo?

29 Aisee, nataka kuwaulizeni jambo fulani hapo. Bado mnakumbuka jinsi alivyomrudishia watoto wake? Sasa, kumbukeni, Yeye alimpa lundo maradufu. Kwanza alikuwa na maelfu mengi ya maksai; wakati wote walipochukuliwa, aliwazidisha hao maksai maradufu. Wakati kondoo, Yeye aliwazidisha kondoo maradufu. Lakini kumbukeni, alikuwa, naamini walikuwa, saba ama kumi na wawili, nasahau sasa walikuwa ni wangapi, wana na binti. Lakini, alikuwa na idadi ile ile ya wana na binti, Mungu alimpa. Je, hiyo ni kweli? Mnaona, aliongeza maradufu kiwango chake chote cha mali, hapa duniani. Sasa, lakini wanawe na bintize, wote waliuawa, lakini Yeye alimpa idadi ile ile ya wana na binti. Je, mliona? Mliwahi kuwazia hilo? Mnakumbuka tulipolifundisha? Mnaona?

30 Hao wana na binti walikuwa wapi? Utukufuni, wakimngojea. Mnaona? Alimpa yeye, kila mmoja wao. Mnaona, hapakuwa na hata mmoja wao aliyepotea. Mnaona? Idadi ile ile ya watoto wa kiume na wa kike aliyoelezea kwanza, alielezea idadi ile ile hatimaye. Lakini Yeye alizidisha idadi yake ya kondoo na ng'ombe maradufu, na kadhalika, namna hiyo. Lakini wanawe na bintize wote waliokolewa, wakingojea, Utukufuni, Ayubu aje kwao. Loo, jamani! Hiyo inastahili yote, sivyo? Vema.

31 Kitabu cha Waebrania. Paulo, kwa maoni yangu, Paulo akizungumza na Waebrania, akitenganisha torati na neema. Na tulikuwa na. . .Labda tutasoma tu vifungu kadhaa, vya—vya vifungu vya kwanza vya mlango wa 10. Kisha tutaanza, hata hivyo, kwenye cha 19. Nafikiri sisi. . .Hebu tuone.

> *. . .torati ikiwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile. . .wanazotoa* kwa. . .*mwaka baada ya mwaka daima haiwezi wakati wo wote kumkamilisha* a—akaribiaye.

32 Sasa, nadhani, ikiwa tutainyosha sehemu hii ya kwanza vizuri, Paulo anajaribu kuwaambia, kwamba torati za kale

zilikuwa kivuli cha mambo mapya yajayo. Sasa, wao, kivuli ni kitu . . .

33 Kama ungeenda kuelekea ukutani, au *huku*, dhidi ya taa, ungegundua kwamba kivuli chako kinaenda mbele yako. Kama ulikuwa ukielekea kwenye machweo ya jua, kivuli chako kingekuwa nyuma yako.

34 Sasa angalieni, "Torati yote ikiwa na kivuli cha mambo yajayo." Mnaona, ni kivuli tu. Sasa, chini ya kile kipindi cha kale cha wakati, Paulo alikuwa akijaribu kusema jinsi walivyotahiriwa, wanaume, kwa mwili, ilikuwa ni mfano wa kutahiriwa kwa moyo, kwa Roho Mtakatifu wa siku hizi. Jinsi walivyozishika amri kule nyuma, ambazo ziliandikwa kwenye vibao vya mawe. Katika siku za mwisho, Mungu alisema angeziandika juu ya vibao vya mioyo yetu ya nyama.

35 Sasa, njia pekee huko nyuma, walijua ilikuwa ni kosa . . . "Usiibe." Ilibidi waione kwenye zile amri. Nayo torati ikaongezwa, kuleta—kuleta upatanisho. Kwa sababu, kama hakuna sheria, vema . . . Kama kuna—kama hakuna sheria, hakuna dhambi. Kwa sababu kama si kosa . . .

36 Iwapo hakuna sheria katika mji huu, inayosema huwezi kupita taa nyekundu, huwezi kufanya *hivi*; mbona, kama ukivuka taa nyekundu, hujafanya kosa, kwa sababu hakuna sheria inayosema hivyo.

37 Kwa hiyo sheria ilileta ghadhabu, au iliweka dhambi wazi. Mnaona, hawakuwa na . . . Walifanya mambo hayo yote nyuma chini ya . . . kabla ya sheria, nayo hayakuwa dhambi kwa sababu hapakuwa na sheria ya kusema kwamba yalikuwa ni dhambi. Lakini sheria ilipokuja, sheria iliongezwa mpaka ukamilifu ulipokuja.

38 Sasa, mwanadamu daima amejaribu kutafuta kitu cha kujiokolea. Bado anafanya jambo lile lile siku hizi; hajashindwa kamwe.

39 Huko India, juma lililopita, kulikuwa na watu waliokuja ambao walikuwa vipofu kabisa, wakiliangalia jua, wakijaribu kupata amani kwa nafsi zao. Baadhi yao wakiwa na kucha zao zilizotokezea sehemu ya nyuma ya mikono yao, namna *hiyo*, wakijaribu kutafuta amani kwa nafsi yao. Kasema kamwe hawataushusha mkono wao, naye alikuwa ameuinua juu kwa muda wa miaka arobaini, akijaribu kupata amani. Wengine miguu yao karibu iteketezwe, pale walipopitia kwenye makaa ya moto, kujaribu kutafuta amani, kuwatuliza miungu wao. Wanalalia glasi, na ni chupa kuukuu zilizovunjika na kadhalika, wanalalia mbao za misumari na kadhalika, wakijaribu kupata amani. Wala hakuna amani kwao, kwa sababu yote ni ibada za sanamu. Nasi hapa Marekani, hatutavuka barabara, kupata amani kwa nafsi zetu, kwa Mungu halisi, wa kweli na aliye

hai. Hiyo ni kweli. Lakini, mambo hayo yote, hayo mawazo ya kipagani ya mwanadamu!

40 Huko nyuma katika wakati ambapo Mungu aliishusha torati, na iliongezwa ili kutuonyesha kwamba mambo haya yalikuwa ni dhambi. Lakini, sasa, torati hiyo isingeweza kuondoa dhambi. Iliikuza tu dhambi. Mnaona?

41 Kwa sababu, kama hakuna sheria inayosema huwezi kufanya *hivi*, mbona, si. . . Sivyo. . . Kama utafanya au kuivunja hiyo, hiyo. . . Huwezi kuivunja, kwa sababu hakuna sheria ya kuvunja.

42 Lakini sheria inapoanza kutumika, basi dhambi inadhihirika. Ndipo walikuwa. . . Wangesema, "Usiibe. Usizini. Usishuhudie uongo." Mambo hayo yote. Walifanya hivyo hapo awali, lakini isingehesabiwa kuwa ni dhambi, kwa sababu hakuna sheria dhidi yake. Lakini basi sheria ilipoingia, ilimfanya mtu kutambua hawezi kuiba, hawezi kusema uwongo, naye. . . kufanya uzinzi. Na amri zote hukuza tu, lakini hata hivyo torati hiyo haikuondoa dhambi. Ilimfanya tu mtu kujua kwamba ilikuwa ni dhambi.

Ndipo, Kristo alipokuja, Kristo alikuja kuondoa dhambi. Mnaona?

43 Sasa, jambo pekee ambalo sheria ilifanya, walijua ya kwamba kibadala kisicho na hatia kilipaswa kufa kwa ajili ya wenye hatia. Sheria hiyo ilianza huko nyuma katika bustani ya Edeni. Na halafu, sasa, wangetoa kondoo, ama fahali, ama kitu fulani, na kumchinja, kutupa damu juu ya madhabahu, na kadhalika; kwa sababu ilikuwa ni kifuniko, au sadaka ya kibadala. Lakini haingeweza kamwe kuondoa dhambi, kwa sababu hakuna nguvu za kutosha katika maisha ya mnyama ya kufanya upatanisho kwa ajili ya maisha ya mwanadamu, maana maisha ya mwanadamu ni makuu kuliko ya mnyama.

44 Sasa, sisi hapa, tumeketi hapa, usiku wa leo. Pengine sisi ni Wajerumani, Waairishi, na kadhalika, wengine watu weusi. Wao, haidhuru kama wao ni weusi, weupe, wa manjano, au rangi yoyote ile, kutoka kwa mtu mmoja alitoka kila mmoja wetu. Mnaona? Hiyo imethibitishwa kisayansi, kwamba unaweza kwenda sehemu yenye giza sana ya Afrika na kumchukua m—mtu aliye mweusi kuliko wote ambaye ungeweza kumpata, na, kama ulikuwa mgonjwa, angeweza kukupa nyongeza ya damu. Damu yako ni kama yake kabisa. Au, ungeweza kwenda Uchina na kumchukua mtu wa manjano kuliko wote Uchina, naye angeweza kukupa nyongeza ya damu. Unaona? Au, mtu wa kahawia kuliko wote aliyeko India anaweza kukupa nyongeza ya damu. "Mungu, kwa damu moja, alifanya mataifa yote, watu wote." Lakini hakuna mnyama ulimwenguni anayeweza kulinganishwa na damu ya mwanadamu. Mnaona? Damu ya mnyama, kila mmoja wao ni tofauti. Lakini damu ya mwanadamu ni sawa.

45 Sasa kama hilo halichukui wazo la baadhi ya watu hawa wanaozungumza, na wanafundisha shuleni, hapa, kwamba tulitokana na uhai wa wanyama. Ikiwa ndivyo, basi mnyama angeweza kumpa mwanadamu damu. Lakini damu, uhai wa mwanadamu, ni wa namna ile ile. Lakini uhai wa mnyama, baadhi yao ni kama nyoka, ana damu baridi; samaki, yeye ana damu baridi; lakini sasa, dubu, kulungu, au mbwa, au farasi, wao ni aina tofauti. Wala, hakuna hata mmoja wao—hakuna hata mmoja wao ambaye angeweza kupeana damu, mmoja kwa mwingine, kwa sababu wote ni tofauti. Lakini binadamu wote ni sawa.

46 Basi kwa kutolewa kwa damu ya mnyama, ilikuwa ni ki—kibadala tu chini ya torati, mpaka Yesu alipokuja, ambaye hakuzaliwa na mwanamume yeyote. Hakuna mwanamume duniani humu ambaye alikuwa baba Yake. Alikuwa na mama, naye huyo mama alikuwa bikira, bikira Mariamu, msichana wa karibu miaka kumi na minane. Naye Roho Mtakatifu akamtia uvuli, akiwa Mungu Baba Mwenyewe, na akaumba. Yeye Yule aliyeunena ulimwengu ukawa, alinena tu.

47 Mnajua, Jumapili, jinsi tulivyoingia humo. Mungu anapozungumza, haina budi kuwa hivyo. Hakuna njia hata kidogo ya kujiepusha nayo. Mungu anasema, "Iwe," nayo haina budi kuwa. Hakuna kitu. . . Neno Lenyewe! Nalo Neno lilikuwa ni wazo. Mungu, wakati Yeye. . . Kabla. . . Neno ni kutamkwa kwa wazo. Mungu aliliwazia niani Mwake; akalinena likawa.

48 Nasi tuna imani moyoni mwetu, imani ya Mungu moyoni mwetu, na tunaweza kuliona dhahiri. Inakuwa imani, kisha tunainena, nayo inakuwepo, jambo lile lile, maana nia ya Kristo iko ndani ya huyo mtu. Hilo ndilo linalofanya uponyaji, na kadhalika. Unapopata ufunuo huo mkamilifu, yale tu unayofanya, basi unajua jinsi ya kutembea. Ndivyo hivyo, kwa sababu huo ndio mwenendo wa Kikristo.

Sasa, lakini damu ya wanyama haikuondoa dhambi.

49 Ndipo Yesu alipokuja, akiwa Mungu Mwenyewe, akidhihirishwa katika mwili, Damu Yake haikutokana na damu ya mtu mwingine yeyote. Kila mmoja wetu, kila nabii, kila mtu mkuu, alikuwa na damu ya mwanadamu. Lakini Mtu huyu alikuwa na Damu ya Kiungu. Mungu, Mwenyewe, aliumba seli ya Damu.

50 Na m—mtu, wewe, ulitoka kwenye chembe moja ya damu, kama ungewahi kuiangalia chini ya darubini. Niliiangalia, majuma machache yaliyopita. Na—na kule kuwazalisha wanyama, ili wewe. . . au ng'ombe, na makumi ya maelfu ya vijidudu mle. Navyo vijidudu hivyo, chembe ndogo za damu, hupiga, na katika hili, katika mwanadamu wa kawaida.

51 Lakini katika. . . mahali hapa, Mungu Mwenyewe aliumba chembe hii ya Damu, bila tendo lolote la mwanadamu hata

kidogo. Ndipo kutoka hapo akaja Mwanawe Mwenyewe, Kristo Yesu, ambaye Mungu Mwenyewe aliishi ndani Yake, ikimfanya Imanueli duniani. Hiyo ndiyo picha. Hilo ndilo unalopaswa kuamini, upate kuokolewa. Na kisha Yesu, kwa hiari, haikumbidi kufanya hivyo, bali kwa hiari, akiwa na upendo moyoni Mwake kwa wanadamu wenzake, alikufa pale Kalvari na kumwaga Damu hiyo, huku dhambi za ulimwengu zikiwa juu Yake, hata akazipeleka dhambi zetu Kalvari, juu yake Mwenyewe.

52 Sasa sio kile ninachoweza kufanya. Sio kama mimi ni mzuri au la. Ni kama Yeye alikuwa mwema. Siwezi kamwe kuwa mzuri vya kutosha kufaulu. Huwezi kuwa mzuri vya kutosha kufaulu. Ukifaulu kamwe, utasimama katika wema wa Yesu Kristo. Nitakwambia hilo sasa, kwa sababu hakuna kitu kingine unachoweza kufanya.

53 Lakini Mungu alihamisha dhambi zetu zote juu Yake, Naye akafa. Na kwa sababu alikufa akiwa mwenye dhambi, Biblia ilisema, "Nafsi Yake ilienda kuzimu." Hiyo ni kweli. Na alipokuwa huko, aliwahubiria wa—wale waliokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika ule uvumilivu wa siku za Nuhu.

54 "Lakini haikuwezekana kwamba angeuacha mwili Wake uone uharibifu, wala nafsi Yake kuzimu." Na siku ya tatu, alifufuka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Inatuonyesha, kwamba imani yetu inapoungamwa katika Yeye, na tumezaliwa upya kwa Roho, ya kwamba kwa hakika kama vile Yeye alivyotoka kaburini, tutafufuka pia katika kule Kuja Kwake mara ya pili. Loo, ni tumaini kamilifu jinsi gani!

55 Loo, unapoziona dini za dunia na ushirikina wao, na kisha uone mahali ambapo wokovu wetu na tumaini thabiti, lenye msingi juu ya kanuni asili, hata pepo wote wa kuzimu hawawezi kulitikisa. Unaweza kuwaona wakitengeneza uzuri. Dini ya Budha ni dini maridadi, dini ya Baniani ni dini maridadi, lakini, ndugu, hawana Uhai kama uhai uwezavyo kuwa.

56 Uhai uko wapi? Uhai uko katika Damu. Damu ni Uhai. Na huyo ndiye Mtu pekee ambaye angeweza kumwaga Damu ifaayo, kwa maana Yeye alikuwa Damu ya Mungu Mwenyewe. Naye aliimwaga Damu iliyotukomboa mimi na wewe. Na kwa hiyo wokovu wetu uko ndani ya Kristo Yesu, yale aliyotufanyia pale Kalvari. Haijalishi jinsi tunavyokuwa duni, jinsi tunavyokuwa watovu wa uadilifu; jinsi tunavyochafuliwa, tunapotazama Kalvari, kwa moyo wa kweli, na kuziungama dhambi zetu pale Kalvari, hilo latosha. Hiyo ni kweli. Si zaidi ya vile maungamo yako yanavyoweza kutoka mdomoni mwako, mpaka Mungu awajibike kukujibu. Hiyo ni kweli. Loo, ninapoliwazia hilo!

57 Loo, si ajabu Paulo alisema. . .Nilisimama pale chumbani, hivi majuzi, ambapo walimkata kichwa, na kumtupa kwenye mtaro. Niliwazia. . .Hapo awali, alisema, "Ewe mauti, u wapi

uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Mnaona? Hilo linatulia tu. Loo, hilo ndilo ninalopenda kuzungumzia.

58 Sikilizeni, baadhi ya vijana. Mnaweza kuwa wachanga, na hilo linaweza kuwa dhaifu, mpaka kweli hulioni. Lakini ngoja kidogo tu, mpaka umelala hapa hospitalini, daktari anasema una siku mbili za kuishi, au saa mbili. Ngoja kidogo tu mpaka moyo huo uanze kuruka mdundo huo, nawe uyasikie yakipanda kwenye mkono wako. Loo, ndugu, utakuwa unatafuta kwa kila kitu basi. Maisha yote yatakuwaje basi? Imekwisha. Ngoja mpaka nywele zianze kuingia mvi kichwani mwako, nawe utambue ya kwamba unakabiliwa na Umilele usio na mwisho huko; na nafsi hii ambayo sasa inaishi ndani yako, inatoka kama—kama jino linalong'olewa, ikijiondoa kutoka kwako namna hiyo, kuingia mahali fulani ambapo hujui unakoenda. Afadhali ulifikirie tena sasa, na ulitatue sasa. Maana, unaweza kung'olewa, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] hivyo, bila hata nafasi ya kutubu. Kwa hiyo, jiweke sawa, sasa.

59 Hakuna udhuru, kwa Wamarekani. Wapagani hao ku—kutoka Afrika Kusini, na kutoka India, huko nyuma kabisa, watafufuka katika ile Hukumu na kukihukumu kizazi hiki, kwa sababu tunayo Nuru, na Injili, na makanisa, na baraka, na kila kitu hapa, nasi tunakataa kulikubali. Hapo ndipo shida ilipo, rafiki. Sasa, ninasema hilo kwa ghafula, kwa sababu ni kwa manufaa yenu, mnaona, kwa sababu ni lazima ufanye hivyo.

60 Sasa, "Torati kwa kuwa ni kivuli." Loo, ninapowazia hilo, "Torati kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa!" Angalia yale torati iliyoleta. Fungua mlango unaofuata, mlango wa 11 wa Waebrania. Angalia kile Danieli alichofanya chini ya torati. Angalia kile Henoko alichofanya chini ya torati. Angalia kile Musa alichofanya chini ya torati. Basi, kama alikuwa akiishi tu katika kivuli cha upatanisho, kanisa la Kikristo linapaswa kufanya nini leo, na uhalisi wa ufufuo wa Bwana Yesu Kristo? Tunasimama wapi usiku wa leo, enyi marafiki?

61 Ninawaambia, inapaswa kumfanya kila Mkristo afunge silaha. Huko lilisema, "Vaeni silaha zote za Mungu. Na mhakikishe mnaleta dirii ya kifuani, na chapeo, na ngao, na vitu hivyo vyote." Paulo akifananisha na askari anayeenda vitani. Na wakati hila za adui zinapoingia, inua juu ngao yako, toka moja kwa moja ukakutane naye.

62 Sasa, kama torati ingeweza kuleta jambo hilo, uhalisi wa Damu ya Yesu Kristo unapaswa kufanya nini! Wakati barua iliyokufa itafanya hivyo, nguvu za kufufua zinapaswa kufanya nini, na Nguvu, na Roho wa Bwana Yesu Kristo zitaleta nini?

63 Sasa tunapaswa kuja kanisani kwa uchaji wa hali ya juu. Tunapaswa kuingia kanisani kama watakatifu halisi wa

Mungu. Tutembee na kuchukua nafasi zetu, na kuweka nia zetu juu ya Kristo. Tunapaswa kuacha kila kitu cha ulimwengu, namna hiyo. Na ikiwa kweli umezaliwa mara ya pili...Hii inaweza kuumiza sasa kidogo tu, lakini unajua hii ni nyumba ya masahihisho. Kama kweli umezaliwa kwa Roho wa Mungu, hapo ndipo moyo wako ulipo, kwa vyovyote vile. Hiyo ndiyo... Mawazo yako yametia nanga kule. Mnaona? Ikiwa umewahi...

64 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kuamini!"

65 Sasa, ikiwa unaamini sawa! Kama ukikiri tu kwa midomo yako, haitasaidia sana. Lakini kutoka moyoni mwako, kama unaamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, huwezi kuishi maisha yale yale uliyoishi wakati mmoja. Huwezi, kama ukipata mtazamo wa kweli wa Kalvari. Sasa, kama unachukua ovyo ovyo tu, una—unajipumbaza tu.

66 Lakini unapopata kwa kweli mtazamo wa jinsi Yesu alivyokuwa! Loo, jamani, jinsi ningetaka kuhubiri Uungu, Uungu mkuu wa Yesu Kristo! Kama mngaliweza kutambua Yeye alikuwa ni Nani, na yale aliyowafanyia ninyi wanaume na wanawake, mioyo yenu ingepasuka ndani yenu, nanyi mngekuwa tayari kutupa takataka za ulimwengu, mpate kumwishia Yeye. Loo, ni ajabu jinsi gani, na alikuwa Mtu wa namna gani! Ukitambua kujidhili kwa Mungu Mwenyewe, akijifunua Mwenyewe, akishuka, mpaka angeweza kuingia moyoni mwako!

67 Wakati Mungu Baba, katika umbo la Wingu kubwa, aliponing'inia juu ya wana wa Israeli; na alipotulia juu ya ule mlima asubuhi ile, kuandika sheria; mbona, kama mnyama angeugusa huo mlima, hana budi kuchomwa mshale. Alimpandisha Musa juu kwa utakaso tu. Akamweka Haruni chini kabisa ya kilima, aangalie na kulinda kwamba hakuna kitu...Ndipo ile Nguzo ya Moto ilipotua juu ya mlima ule, radi ikitokea, na ngurumo zikavuma, giza likatanda. Wakati Yehova Mungu, Muumba wa Milele yote, alipotua juu ya mlima aliouumba, Mwenyewe, kilindi cha mawingu kikipasuka, kwa radi, tetemeko la ardhi! Mpaka, hao Waisraeli waliosimama kule kambini, huku dhabihu inayotoka damu ikiwa karibu nao, wakasema, "Acha Musa anene, wala si Mungu, tusije tukafa." Wazia hilo.

68 Mwenye Uhai yuyo huyo mkuu, Mwenyezi, alijinyenyekeza na kujifunua Mwenyewe, na kuingia katika mwili wa nyama ambao mtu yeyote angeweza kuugusa kwa mikono yake. Anafanya nini? Akidai njia Yake, akijaribu kuingia ndani ya mwanadamu. Ndipo, baadaye, Yeye alienda akatoa Damu Yake Mwenyewe, ambapo hakuna damu nyingine ingefaa! Si ajabu Yeye alikuwa ni gharama ya Mbinguni yenye gharama isiyopimika! Si ajabu alikuwa Mfalme wa wafalme

wote! Alipojifi-. . .alipojifunua Mwenyewe, na akashuka na kujisalimisha katika mikono ya mwanadamu mwenye dhambi, akapigwe, na kutemewa mate, na kuchubuliwa, na kutundikwa msalabani, na kufa. Alipokuwa amesimama pale, mtu fulani alisema. . .Aliposema, “Ningeweza kumwita Baba Yangu, Naye angenitumia majeshi kumi ya Malaika. Lakini Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu.”

69 Na hapo huo umati wa watu ukasema, “Mwondoshe! Mwondoshe!”

70 Kwa nini hakugeuka na kusema, “Uondoshwe wewe”? Hii hapa sababu asingeweza, marafiki. Iangalieni. Hao walikuwa ni watoto Wake Mwenyewe. Kuwazia, watoto wa mtu wakiililia damu ya baba yao. Kama watoto wangu walikuwa wakiililia damu yangu, kusingekuwako na kitu kingine ambacho ningeweza kusema, “Nichukueni.” Kama—kama alikataa kufanya hivyo, alimpoteza mtoto Wake; uumbaji Wake Mwenyewe, wanadamu Wake. Nao ndio waliokuwa wakiililia Damu Yake. Ungeweza kuwazia watoto wakiililia Damu ya Baba yao? Hiyo ndiyo sababu asingweza kusema la. Kama angesema la, walikuwa wamepotea. Ningekufa kwa hiari kwa ajili ya watoto wangu, na baba mwingine yeyote angefanya hivyo. Angalieni alivyokuwa, watoto Wake Mwenyewe wakiililia Damu Yake.

71 Nayo haki ya sheria ilihitaji Damu. Wala damu ya kondoo isingefanya hivyo, damu ya mbuzi isingefanya hivyo, damu ya ng’ombe isingefanya hivyo, bali ilibidi Damu ya Mungu Mwenyewe ifanye hivyo. Naye Mungu alifanyika mwili, akaishi hapa duniani. Huyo Mtu mkuu aliyenguruma juu ya Mlima Sinai alikuwa hapa katika mwili wakati huo.

72 Kisha akaitakasa njia apate kuja na kuishi moyoni mwako. Na sasa Roho yeye yule, aliyenguruma kutoka Mlima Sinai, anaishi ndani ya moyo wa mwanadamu. Ni ajabu jinsi gani! Jamani, hilo, hilo linapaswa kuufanya kila moyo kuruka, na ku—kuliwazia.

73 Sasa tukipita upesi, Paulo alikuwa akiendelea mbele, hadi kwenye kifungu cha 5 na cha 6 hapa. Tunajaribu kufikia kwenye cha 19, tupate kuharakisha. Cha ku-. . .Cha 5 na cha 6, na kuendelea chini, alikuwa akizungumzia jinsi sheria inavyotanguliza. Jinsi ambavyo katika Agano la Kale. . . Tulilipitia, hivi majuzi. Loo, miezi michache iliyopita, ilikuwa, katika shule ya Jumapili.

74 Mwanadamu yuko chini ya dhambi; tuseme alizini, au aliiba, au kuvunja Sabato, au amri nyingine. Basi ilimbidi kuchukua mwana-kondoo, naye ilimbidi kumleta mwana-kondoo huyu kwa wazee, nao iliwabidi kumchunguza mwana-kondoo huyu. Ilibidi mwana-kondoo asiwe na ila, ilibidi asiwe na dosari juu yake. Angalia umuhimu hapa. Huyo Mwana-kondoo ilibidi

awe bila lawama, kwa mtu aliyelaumiwa. Amina. Natumaini mnaliona. Jamani!

75 Ninakumbuka hadithi ndogo. Sijui kama niliwahi kuwaambia, au la. Ni hadithi ndogo tu ya kubuni, namna hiyo. Ninii. . .Chini ya sheria, kama maskini mama farasi alikuwa na mtoto mdogo, naye alikuwa nyumbu, mwajua, nayo masikio yake yalivunjika, na magoti yake yana magobwe, na, loo, ni nyumbu mwenye sura mbaya jinsi gani na mwenye makengeza. Vema, nyumbu huyo, kama angeweza kujiangalia, angesema, "Loo, jamani! Bwana atakapotokea, ataniua, kwa sababu mimi. . .Hatanilisha. Sistahili kuishi. Niangalieni, jinsi ninavyonekana wa kuchukiza!"

76 Lakini kama huyo mama angeweza kumjibu maskini huyo jamaa mdogo, angesema, "Ngoja kidogo, mpenzi! Unaweza kuishi, kwa sababu wewe ndiye kifungua mimba wangu, na una haki ya mzaliwa wa kwanza. Sasa bwana akitokea na kukuona katika hali yako yote, hana budi kurudi na kumchukua mwana-kondoo asiye na ila juu yake, na kumchinja, ili kwamba nyumbu huyo anayeonekana mlemavu aweze kuishi." Mnaona, kuhani kamwe hakumwona yule nyumbu; alimwona mwana-kondoo. Haikuwa kama huyo nyumbu alikuwa mkamilifu; ilibidi awe mwana-kondoo mkamilifu.

77 Loo, natumaini mnaliona. Sio kama wewe ni mzuri vya kutosha kuwa Mkristo au la. Ni kama Yeye alikuwa mzuri vya kutosha. Kama Mungu alimkubali, nayo Damu Yake inafanya upatanisho, Mungu hakuoni; anamwona Mwana-Kondoo. Loo, jamani!

78 Basi maskini huyo nyumbu angeweza kunyoosha mkia wake hewani, na kukoroma, na kuruka, na kukimbia huku na huko shambani, awe na wakati mzuri. Ataishi. Lakini mmoja, mkamilifu, ilibidi afe kwa ajili ya wasio wakamilifu.

79 Huyo alikuwa ni mimi, William Branham; sifai kitu, sistahili kuishi, nastahili kwenda jehanamu; nilizaliwa katika familia yenye dhambi, nikalelewa mwenye dhambi; si mwema hata kidogo, hakuna sehemu moja ya maana kunihusu. Hiyo ni kweli. Lakini, siku moja, nilikubali! Haleluya! Wakati Mungu alipoinama akamwangalia Kristo, naye Kristo akapachukua mahali pangu, basi Mungu hanioni; anamwona Yeye aliye Mkamilifu. Basi mradi niko humu ndani, ndani Yake, basi nimekamilishwa; si ndani yangu. Katika Yeye; sio ukamilifu wangu! Sina wowote; huna wowote. Lakini ni ukamilifu Wake.

80 Kwa hiyo, Yesu hakukosea aliposema, "Basi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Basi mwanadamu angewezaje kuwa mkamilifu? Angeweza kuwa mkamilifu kwa imani yake kamilifu, ikitulia ndani Yake, akisema, "Alilipa gharama kwa ajili yangu."

Yesu alilipa yote,

Na yote Kwake ninawiwa;
Dhambi ilikuwa imeacha doa jekundu sana,
Akaliosha likawa nyeupe kama theluji.

81 Jamani, hilo hutufanya sote Methodisti wanaopaza sauti, sivyo, unapowazia jambo hilo? Wewe. . .Ninaliamini. Ninaamini katika tukio la mtindo wa kale la kupaza sauti. Naam, bwana. Kama watoto wakipata aina nzuri ya vitamini, daima wanajisikia vizuri, unajua. Mnajua ninachomaanisha. Tunahitaji vitamini za kiroho makanisani leo. Sivyo?

82 Inanikumbusha juu ya mkulima, wakati mmoja. Alikuwa na ninii kidogo. . .Huyo mkulima mmoja, alikuwa na ki—kibanda, naye alikuwa na zana zote nzuri za kulima zi—zi—zilizompasa kulima nazo, matrekta na kadhalika. Lakini, alikuwa mvivu sana kulima, kwa hiyo a—aliachilia sehemu yake imee magugu. Basi wakati wa majani kupukutika ulipowadia, jambo pekee la kufanya, ni kukata magugu yake na kuyaweka ghalani.

83 Ndipo kulikuwa na mkulima mwingine, hakuwa na ghala la kupendeza sana, lakini alikuwa. . .Alikuwa mtu mwerevu. Basi akatoka, naye alikuwa mwenye bidii. Naye angefanya kazi, maana alitaka kulisha mifugo wake. Akavuna karafuu nzuri, na alfafa, akaziweka ghalani.

84 Katika mashamba yote mawili, kulikuwa na ndama mdogo aliyezaliwa kila mwaka, mwaka huu. Na, wakati, yule ndama mdogo kule kwenye banda lingine, alilazimika kulishwa magugu, lakini alikuwa na banda zuri maridadi. Naye maskini yule ndama mwingine hakuwa na banda linalofaa, lakini alikuwa na kitu cha kula.

85 Hiyo inanikumbusha baadhi ya maskini makanisa haya ya kale, anaangalia maeneo yake makuu, makubwa, marefu, ya kutamanisha, mnajua, na vinanda vya paipu vya dola elfu moja, maelfu, nilimaanisha, na viti vya kifahari na kila kitu kizuri sana. Lakini je, kuna chochote cha kula? Hilo ndilo jambo linalofuata.

86 Unaingia katika misheni fulani ya kale mahali fulani, unajua, na unaweza kupata mengi mle ndani, unajua, baadhi ya vitamini za kiroho. Mungu anazo kwa ajili yako, za kuichochea roho yako, kukuinua kidogo. Huko ni kuihubiri Injili. Haleluya! Kama huko hakutaliamsha kanisa, hakuna kitakachoweza. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.”

87 Ninaposikia Yesu alikufa kwa ajili yangu, nasema, “Hilo latosha. Utukufu kwa Mungu! Niko salama sasa kwa sababu niko ndani Yake.” Alinikubali. Hiyo ni kweli. Alinichagua mimi. Alikuchagua wewe. Kila mmoja wenu hapa ndani, ambaye ni Mkristo, Yesu alikuchagua. Ni yako. Sawa. Alikuchukua.

88 Ndama huyu mdogo, mmoja wao, alikuwa amebingirika, alikuwa kwenye zizi hili kubwa zuri, na rafu za karati kumi na nne, mwajua, na vibanda na kadhalika. Alipotoka nje, maskini

jamaa huyo alitoka akitembea kwa shida, mwajua. Alikuwa amekonda sana; akila magugu majira yote ya baridi kali. Kwa hiyo huyo mwingine. . . Alitoka eneo hilo la banda, mwajua, na upepo wa joto ukivuma, na kidogo. . . upepo karibu umbwage chini; alikuwa dhaifu sana.

89 Ndipo huko upande wa pili, mkulima huyu akamtoa maskini ndama wake, na, loo, alikuwa mnene na mduara, mwajua. Jamani, alikuwa katika hali nzuri. Alipofika pale, alianza tu kuruka-ruka, kuchezacheza, mwajua, alikuwa na wakati mzuri, mkutano mkubwa wa kipentekoste, akirukaruka tu pale.

90 Mnajua maskini ndama huyo alifanya nini? Yule kwenye ghala kubwa, alikuwa na vitu vyote vikubwa, mwajua. Akaangalia chini, akachungulia kwa jicho lake dogo kwenye ufa, akasema, "Tsk, tsk, tsk, tsk! Ulokole wa jinsi gani! Ulokole wa jinsi gani!"

91 Maskini jamaa huyo mdogo alikuwa akijisikia vizuri, si ajabu angeweza kuruka. Alikuwa amenenepeshwa. Alijisikia vizuri.

92 Hiyo ndiyo njia wakati mtu anapopata vitamini zake za kiroho. Nyumba ya Mungu, ije pale, na nafsi yake imelishwa Neno la Mungu, ambapo anajua anaposimama. Ushirikina wake wote wa kale unatoweka. Na ibada za ibilisi na chochote kile, zinatawanyika tu, unapoona ya kwamba Yesu Kristo alikufa badala yangu, akapachukua mahali pangu pale Kalvari. Upendo safi wa Kiungu, unakuja hapo. Inanifanya nikose adabu, kwa ulimwengu, mara kwa mara. Ninajisikia vizuri sana kulihusu, kwa sababu ninajazwa tu na vitamini, hivyo ndivyo, vitamini hizi nzuri za kale *Hapa*.

93 Sasa, Paulo alisema, wakati mwabuduo alipokuja na kuleta maskini. . . Kama alifanya makosa, alikuja pamoja na maskini mwana-kondoo huyu. Sasa kuhani mkuu akamchunguza, kuhani akamchunguza, na akaona hakuna kasoro kwa mwana-kondoo huyo. Akamchunguza, aone kama alikuwa sawa, na, kama alikuwa sawa, basi akamlaza maskini huyo mwana-kondoo mdogo madhabahuni.

94 Basi huyu hapa akaja mtu aliyefanya makosa, akasema, "Sasa, nimekuwa nikiiba. Nami sasa najua ya kwamba ninapasiwa kifo, kwa sababu nimefanya makosa. Mungu asingetaka niibe; amri Yake inasema nisiibe. Sasa nitaweka mikono yangu juu ya maskini mwana-kondoo huyu. Nazo amri za Mungu hapa zilisema, 'Usiibe,' nami nimeiba. Kwa hiyo mimi. . . Najua ninapasiwa mauti. Kitu fulani hakina budi kuwajibika kwa ajili ya dhambi yangu, maana niliiba. Ndipo Mungu akasema, siku nitakapokula, siku hiyo nitakufa. Kwa hiyo, niliiba. Naye Mungu alisema, 'Umeiba, huna budi kufa kwa ajili yake.' Kwa hiyo alihitaji, kama sikutaka kufa, ilinibidi kuleta mwana-kondoo. Kwa hiyo nikamlaza mwana-kondoo

hapa chini, nami ninaweka mikono yangu juu ya kichwa cha maskini jamaa huyu, huku yeye akilia tu na kuendelea. Nami nasema, 'Bwana Mungu, nasikitika kwamba niliiba. Ninakiri na kukuahidi sitaiba tena, ikiwa utanikubali tu sasa. Na kwa ajili ya dhabihu yangu, na kwa kifo changu, maskini mwana-kondoo huyu atakufa badala yangu.'"

95 Ndipo wakachukua ndoana kubwa na kuiweka chini ya maskini koo lake, na kuikata namna *hiyo*; wanamnyanyua *hivi*, na maskini jamaa huyo analia, akilia. Sufi ikiruka, yote imelowa damu namna hiyo. Na maskini kinywa chake, naye akilia, akilia, akilia. Basi muda si muda mwajua, damu yake inadondoka inakwisha, naye anainamisha maskini kichwa chake. Ni hayo tu.

96 Halafu, mtu huyo, imeandikwa hapa kwenye kumbukumbu, anawekwa kando ya lile sanduku, namna *hii*, kwamba mtu huyo alifanya maungamo. Kama akifanya hivyo mara ya pili, katika mwaka mmoja, hana budi kufa kwa vyovyote vile; hana budi kufa pamoja na mwana-kondoo.

97 Sasa, hilo lilikuwa ni Agano la Kale. Alirudi moja kwa moja kutoka pale, mara alipofanya maungamo yake, akarudi moja kwa moja. Na labda akazini. Labda alikuwa amefanya kosa fulani, mengi zaidi . . . ? . . . Aliporudi kutoka pale . . . Labda alimwua mtu. Labda . . . Aliporudi huko nje, kwa vyovyote vile, alienda pamoja na jambo lile lile moyoni mwake, alilofanya alipoingia. Hakuna mabadiliko ndani yake; ila tu yeye, kwa sheria, andiko la sheria, alitimiza masharti. Sasa, hilo halingeweza kumfanya, lisingeweza kuubadilisha moyo wake. Kitu pekee alichojua, "kilikuwa ni makosa," kwa maana alilisoma kwenye torati, naye mwana-kondoo akafa mahali pake. Sasa, Yesu alipokuja, mnaona, Damu ya Kristo . . . Mnaona, hiyo damu iliyomwagika ilikuwa ya aina gani? Damu ya mnyama. Uhai wa mnyama, kwa maisha ya mwanadamu, hauwezi kabisa kuondoa dhambi; hauwezi!

98 Sasa Yesu alipokuja, haukuwa uhai wa mwanadamu tu, bali ulikuwa ni Uhai wa Mungu Mwenyewe, Mwenyewe. Huo ndio uliokuwa katika Damu Yake.

99 Sasa, tunaona kwamba tunatenda maovu, "Loo, nimefanya kosa. Nimefanya dhambi. Ni—nimeishi vibaya. Nimefanya kosa." Sasa naja madhabahuni. Kwa imani naiona Dhabihu; ninaweka mikono yangu juu ya kichwa cha Yesu. Nasema, "Mungu mpendwa, najua kwamba ninii zangu . . . Mimi ni mwenye dhambi, na mshahara wa dhambi ni mauti. Na ikiwa nimefanya kosa, sina budi kufa. Na kama nikifa, siwezi kuja Mbele Zako, nitaadhibiwa katika mateso milele na milele. Kwa hivyo, nimekosea, Baba. Nami ninataka kuwa sawa, wala sitaki kufa namna hii." Kwa hiyo, ninaweka mikono yangu juu ya kichwa Chake, na uhai Wake ukachukuliwa kwa ajili ya uhai

wangu. Lakini jambo ni kwamba, ninapoondoka madhabahuni, ninaondoka nikiwa na moyo uliobadilika. Mnaona?

100 Mtu wa kwanza aliondoka, chini ya sheria, chini ya damu ya mnyama. Haingeweza kuubadilisha moyo wake, kwa sababu uhai wa mnyama hautalinganishwa na uhai wa mwanadamu. Mnyama hawezi kumpa damu mwanadamu. Mnaona? Mnyama hawezi kufanya hivyo, kwa sababu uhai wake ni uhai tofauti. Na mnyama ana uhai, lakini sio nafsi. Mnyama ni kiumbe hai, lakini sio nafsi.

101 Lakini Mungu aliweka nafsi juu ya mwanadamu. Kwa hivyo, basi, nafsi yangu . . . Nafsi ni nini? Tabia ya roho.

102 Basi nafsi ya Kristo ilipoachwa, haikuachwa kuzimuni, bali ilitwaliwa juu; kupitia kwa Damu, kumwagwa kwa Damu Yake, wakati Mungu alipompeleka Kalvari. Ilichanganya Damu Yake pale msalabani; na aliposimama pale, akitikisa kichwa Chake huku na huko, taji kichwani Mwake, namna *hii*, pamoja na miiba, Damu ikitiririka usoni Mwake, ikichuruzika kutoka kwenye vishungi vya nywele Zake, mabegani mwake, akilia kwa lugha zisizojulikana, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Huyo hapo Mwana-Kondoo. Huyo Ndiye.

103 Huyo Ndiye asiye na hatia aliyekufa; ili mimi, nisiyestahili, nifanywe sawa, ili nipate kuwa na haki ya Uzima. Huyo ni asiyestahili—asiyestahili . . . wewe ndiwe asiyestahili ambaye Mwana-Kondoo alimfia. Sasa njoo hapa na uweke mikono yako juu Yake, unaona, na kufanya maungamo yako, naye Mungu anakujibu kwa Roho Mtakatifu, kama thibitisho kwamba amekupokea.

> . . . kwa dhabihu *moja* (hii hapa), *kwa* dhabihu *moja amekamilisha hata milele* . . .

104 Haya basi. Kwa maana mwabuduo akija kila mwaka, ilikuwa ni jambo linaloendelea, karibu kila mwaka, alirudi; nawe ulipaswa kuja mwaka uliofuata, tamaa ile ile moyoni mwake. Bali alipotoa Dhabihu moja, Mwenyewe, kila dhambi, kila tamaa ya dhambi, na kila kitu kilichukuliwa kutoka kwa moyo wa mwanadamu. Naye anasimama mkamilifu machoni pa Mungu, si kwa yale aliyofanya, bali yale Yesu aliyomfanyia. Naye aliikubali Sadaka ya Bwana Yesu Kristo. Loo, ni mambo ya ajabu jinsi gani, rafiki!

105 Sasa, "Kwa kuwa . . . " Sasa kifungu cha 19. Tuna kama dakika ishirini, hebu tuweke yote katika Maandiko sasa. Sasa kifungu cha 19.

> *Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu,*

106 Sikilizeni, hili hapa, "Sasa kupaingia Mahali Patakatifu Sana." Kuna mahali patakatifu, kisha Mahali Patakatifu Sana. "Patakatifu pa patakatifu," paliitwa. Kuhani mkuu aliingia

mara moja kwa mwaka. Na alipofanya hivyo, jambo la kwanza alilopaswa kufanya lilikuwa ni kunyunyiziwa, yeye mwenyewe. Sanduku lilikuwa huko nyuma ya pazia.

107 Naye kuhani mkuu ilibidi atiwe mafuta kwa manukato yaliyotengenezwa kutoka kwa Ua la Uwandani. Hakuna manukato mengine yangefanya. Je, unajua Yesu aliitwa Ua la Uwandani? Ua ni nini? Manukato hutoka wapi? Kutoka kwa waridi. Ni wapi . . .

108 Yesu aliitwa Ninyoro ya bondeni. Je, hiyo ni kweli?

109 Kuna mtu anayejua afyuni hutoka wapi? Kutoka kwa ninyoro. Afyuni huletwa kutoka kwa ninyoro. Na afyuni hufanya nini? Afyuni hupunguza maumivu. Wakati watu ni wagonjwa na, wakiteseka sana, wanarukwa na akili, wazimu, wanawandunga afyuni, na hilo latosha. Wanatulia. Hiyo ni katika mambo ya kimaumbile.

110 Yesu, katika mambo ya kiroho, ni Ninyoro ya bondeni. Na unapofikia mahali kama hapo, huwezi kuvumilia tena, na maisha hayana maana kwako, Mungu ana sindano ya afyuni kwa ajili yako, kutoka kwa Ninyoro ya bondeni, ambayo inakupunguzia shida zako zote, zote zimetoweka. Haikubidi kulewa wiski, upate kupunguza shida yako; zitarudi moja kwa moja tena. Lakini njoo upate ki—kinywaji cha afyuni kutoka kwa Ninyoro ya bondeni, nazo zimeisha milele.

111 Yaje, yaende, yatakavyo; uishi, ufe, kama wewe ni *hiki*, ama *kile*, ama *kinginecho*; hakuna kitu kinachokutenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu. Wakristo hawajaahidiwa kitanda cha maua cha anasa, lakini wameahidiwa neema ya kutosha kwa kila hitaji walilo nalo. Amina. Aisee, ninaamini ninajihisi kubarikiwa sasa hivi. Wazia hilo! Naam, bwana. Maana, ninapochoka, na kushangaa, ninaangalia hapa na kuona *haya* yakiendelea, *yale* yakiendelea, lakini nawazia, "Hebu kidogo. Jamani, jamani!" Mnaona? Yule pale Ninyoro ya Bondeni.

112 Sasa, hiyo harufu inafanya nini? Harufu, wanawake hujipaka manukato wapate kuvutia. Nao wanaume hujipaka manukato baada ya kunyolewa, wakati mwingine, namna hiyo; kusudi harufu, harufu mbaya, ziondolewe kwako. Unapotembea mbele ya mtu, ukiwa na harufu ya mwili au na kitu kingine, manukato ni ya kuondoa harufu hiyo; ili wewe, mbele ya mtu huyo, usinuke vibaya. Haivumiliki. Hayo ndiyo manukato au . . . Sabuni ina harufu ndani yake. Nawe ukioga kwa sabuni, au poda ya ulanga, ama chochote kile, hiyo ndiyo sababu wanaitumia.

113 Sasa angalieni. Amina. Najisikia tu vizuri. Angalieni. Yesu alisema . . . Mnaona, Yeye alikuwa Ua la Uwandani, Naye akatolewa kwa Mungu kama Harufu ya kupendeza. Na hii . . . Na ndipo tunapokuwa wasiovumilika mbele za Mungu, na kwa

hivyo, kunradhi hili tamshi, kuvunda sana, mnaona, hata dha—dhambi zetu na kadhalika ni mbaya sana na zinavunda sana, ndipo tunakuja Kalvari na ambapo. . .

114 Ninyoro, au ua lolote, kabla ya kutengeneza manukato. . . Unachukua ua, linapendeza; ninyoro kubwa ya asubuhi, au waridi. Ua la Uwandani ni ua la kupendeza. Wakati likiwa hai, linapendeza. Lakini ili kupata harufu kutoka kwa hilo, kupata manukato, halina budi kupondwa-pondwa. Na wanaliponda na kukamua manukato kutoka kwake.

115 Mnaona, Kristo, alipokuwa hapa duniani, alikuwa mzuri. Aliponya wagonjwa. Aliwafufua wafu. Maisha Yake hayakulinganishwa kamwe. Alikuwa wa kupendeza. Bali kukufanya kama Yeye alivyokuwa. . .Mungu alipoangalia chini, alisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa Naye." Kasema, "Dhabihu zenu zinanuka chini ya pua Yangu, lakini Huyu Ndiye anipendezaye." Sasa, Yeye alipendezwa sana.

116 Na kutufanya tuwe tunapendeza sana kwa Mungu, ilimbidi apondwe pale Kalvari, nayo dhambi ya ulimwengu huu ilibidi kuusonga uhai, kutoka Kwake. Naye akafa, akizibeba dhambi za ulimwengu, tupate kutiwa mafuta na Ua la Uwandani. Alikuwa Ninyoro ya Bondeni. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu," Harufu nzuri ya kupendeza. "Kwa kupigwa Kwake wewe uliponywa," Ninyoro ya Bondeni ambayo hutupa afyuni, ili kutuliza magonjwa na maumivu yetu. Ni picha ya ajabu jinsi gani!

117 Sasa, kuhani mkuu, kabla hajaingia hapo Patakatifu pa patakatifu, jambo la kwanza, ilimbidi avae vazi fulani lililotengenezwa. Lisingeweza kushonwa na mtu yeyote; ilibidi lishonwe kwa mkono mtakatifu. Hiyo ilionyesha kwamba mavazi yetu. . .

118 Hii hapa! Mimi. . .ilitokea tu kwamba lilinijia wakati huo. Ndugu, kama umevaa tu vazi la kanisa, afadhali ukiondoloee mbali kitu hicho; huwezi kwenda nyuma ya Patakatifu pa patakatifu. Vazi ambalo kuhani mkuu alivaa mle ndani, ilibidi lishonwe kwa. . .kwa mkono mtakatifu, kitambaa kilichochaguliwa, amina, kikateuliwa na Mungu. Hiyo hapo. Kwa hiyo kama ulijiunga na kanisa na kudhania uko sawa, umekosea. Unaona? Inabidi liwe vazi lililochaguliwa na Mungu. Wala matambara yetu ya kujihesabia haki hayatasimama Mbele Zake. Inahitaji Roho Mtakatifu, ambaye ndiye vazi la Mungu ambalo humvalisha mwaminio apate kwenda nyuma ya Patakatifu pa patakatifu. Loo, hilo ni zuri. Nalipenda hilo. Hilo lilikuwa jipya. Sijawahi kumeza moja kama hilo hapo awali, lakini, ndivyo hivyo, aina hiyo tu, hiyo ndiyo vitamini halisi. Mnaona? Inahitaji Ro—Roho Mtakatifu!

119 Angalia katika mfano wa. . .Alikwenda kwenye karamu ya arusi, na kila mtu katika karamu ya arusi ilibidi avae vazi

fulani. Ndipo akakutana na mtu huko ambaye hakuwa na vazi la aina hiyo. Naye akasema, "Rafiki, unafanya nini hapa? Uliingiaje?" Sasa, mnaona, kama mnaujua huo mfano. Katika nchi za Mashariki huko, katika nchi ya Mashariki, wanapofanya arusi, mpaka wa leo, bwana-arusi hana budi kumwalika yeyote atakaye.

120 Naye Mungu anaweza. . . "Hakuna mtu awezaye kuja kwa Mungu, au kuja kwa Kristo, asipoitwa na Mungu kwanza." Mnaona, ni uteuzi, wa Mungu. Sasa angalieni kwa makini.

121 Na kisha bwana arusi, ikiwa ametoa huo mwaliko, hana budi kuleta hayo majoho. Wala hakuna mtu. . . Kwa sababu, anawaalika maskini, anawaalika matajiri. Lakini kufanya kila mtu aonekane sawa, hana budi kuvaa vazi la aina ile ile, alilo nalo maskini, na alilo nalo tajiri. Mnalipata?

122 Sasa, Mungu anapompa fukara Roho Mtakatifu, ni Roho Mtakatifu yeye yule anayempa tajiri. Mnaona, wote hawana budi kuwa sawa. Ili kwamba, wanapokuja Mbele za Mungu, hakuna mtu anayeweza kusema, "Nimevaa vizuri zaidi," kwa sababu ni Damu ile ile, neema ile ile, Roho Mtakatifu yeye yule, akiwafanya mtende vile vile. Tajiri na maskini hawana budi kufanana. Huo ndio ule mfano hasa. Angalieni.

123 Na kisha wanapokuja na mwaliko wao, wao. . . Mavazi yalitolewa mlangoni. Yule mtu akasimama pale; akaonyesha mwaliko wake, kwamba amekuja kisha anauwasilisha. Wanafanya hivyo nchini India, hivi sasa. Na, kwa hiyo, wanakuja kwenye harusi. Bawabu amesimama pale mlangoni, mwenye nyumba, nawe unatoa mwaliko wako. "Naam, bwana." Watarudi hapa nyuma, wachukue joho, joho tu, na kumvika. Anaingia ndani. Hiyo inaonyesha kuwa amealikwa rasmi, amekubalika rasmi, na sasa yeye ni mwanachama. Amina. Haya basi.

124 Sasa Mungu Baba, Roho Mtakatifu, anatoka na kukupa mwaliko wa Karamu ya Arusi. Unaona? Sasa, ni juu ya Bwana-arusi, basi, kuandaa hayo majoho. Naye aliyaandaa, kwa Uhai Wake Mwenyewe, akitoa Roho Mtakatifu. Nawe unakuja mlangoni, amina, pamoja na mwaliko wako. Yesu alisema, "Mimi ndimi mlango wa zizi la kondoo." Basi unapokuja kupitia Jina la Yesu, unapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Je, hiyo ni kweli? Unampokea Roho Mtakatifu, kisha unaingia, nawe unakuwa mshiriki, mshiriki wa familia ya Mungu. Mwanachama!

125 "Unasema, 'Ati mwanachama'?" Hakika. "Je, nitakuwa mtumishi?" La, sivyo.

126 Unakuwa mwanachama. Nyinyi si watumishi. Ninyi ni wana na binti. "Sisi sasa ni wana na binti za Mungu," mwenyeji wa familia ya Mungu. Jamani, loo, jamani! Huenda nikaishi katika kibanda, lakini mimi ni Damu ya Kifalme. Haya basi. "Mwenyeji wa nyumba ya Mungu." Hayo ni Maandiko. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema. "Ni upendo wa namna gani ambao

Baba ametupa, mnaona, kwamba tuitwe wana wa Mungu!" Loo, jamani! Hao hapo, uanachama.

127 Sasa, kuhani mkuu, akitiwa mafuta, akiingia, ilimbidi aende pamoja na damu ya mnyama, la sivyo angekufa.

128 Na jambo jingine, kuhusu vazi lake. Je, mlijua, mwishoni mwa vazi hilo, mlipata kujua kilichokuwa nchani mwake? Alikuwa na kitu fulani nchani mwake. Na kila. . .Kilikuwa kitu kidogo kinachoning'inia, nchani mwa upindo wa vazi lake, nacho kilikuwa ni komamanga na kengele, na komamanga na kengele.

129 Naye ilimbidi atembee kwa njia fulani alipoingia. Asingeweza kupiga tu hatua zake kwa njia yoyote ile. Ilibidi atembee kwa namna fulani. Kwa maana, kila alipopiga hatua, kengele hizo zilipaswa kulia, zikigongana na hayo makomamanga, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana." Ndipo Bwana akamsikia akikaribia. Amina. Haleluya!

130 Hiyo hapo. Mungu hukusikia ikiwa unakuja kwa njia iliyowekwa na Mungu unapomkaribia, kwa maana unakuja, ukilia kutoka moyoni mwako, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi." Hapo unaingia, hata hivyo, unapokuja, ukimtafuta Roho Mtakatifu. Unaona? "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi."

131 Na halafu, kusanyiko, njia pekee waliyojua. . .Sasa, kama uliingia mle, bila kuvaa vivyo hivyo hasa, angeninii, angekufia m—mlangoni. Hakutoka tena. Alifia mle ndani, kama hakuingia, amevaa na kupakwa mafuta aingie. Sasa. . .njia pekee ambayo kusanyiko lilijua kama alikuwa sahihi, ama la. Loo, jamani! Njia pekee ambayo kusanyiko linalongojea lilijua kama kuhani mkuu alikuwa sahihi, au la, walisikia mlio wa kengele hizo. Kulikuwa na kelele mle ndani, na hivyo ndivyo walivyojua kama alikuwa sahihi, ama la.

132 Nashangaa kama jambo lilo hilo linafanya kazi siku hizi. Ukipitia kwa kanisa, na kila kitu kimekufa tu na kutulia, sijui mimi. Lakini anapiga kelele, mwajua, anawafanya watu wajue ya kwamba Mungu angali juu ya Kiti cha Enzi, Mungu hujibu maombi, watu bado wana Roho Mtakatifu; wakipiga kelele za sifa za Mungu, wakimtukuza Mungu, wakipiga kelele nyingi. Kusanyiko linasema, "Vema, hapana shaka yuko karibu hapa. Hapa ni mahali hai." Tunapoingia Patakatifu pa patakatifu, na kudai kuwa Wakristo, lazima kuwe na kelele. Simaanishi kidogo, upuuzi mwingi. Namaanisha kelele halisi, za kweli. Hiyo ni kweli. Sasa angalieni hapa.

> *Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu,*
>
> *Kwa njia mpya iliyo hai,* si sheria ya kale, wakati yeye amepatanisha kwa ajili ya. . .*ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake;*

*Na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu;*

*Na tukaribie wenye moyo wa kweli,* na kwa *utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo . . . dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.*

*Na tushike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; (kwa maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu;)*

133 Hiyo inaondoa tu yote. Loo, jamani! Ninapenda hili, lakini nadhani inatubidi kufunga. Lakini tunapokwenda mbele za Mungu, hebu tusiende, tukisema, "Naam, sasa, nashangaa tu kama kila kitu kiko sawa. Mimi—mimi . . . " Je, wewe ni Mkristo? "Vema, na—natumaini ndivyo." Hiyo siyo njia ya kuja.

134 Ndugu, amini hiyo hadithi! Ikubali, na uzaliwe mara ya pili. Ndipo utembee kwa imani safi, ukijua hili, ya kwamba, Mungu ameahidi, naye Mungu hawezi kusema uongo. "Mungu aliniahidi Uzima wa Milele, kama ningemwamini Mwanawe, Yesu Kristo. Niliamini; Naye akanipa Uzima wa Milele."

135 Nilifanya makosa mengi, bado ninayafanya, sikuzote nitayafanya. Lakini, ninapoyafanya, Roho Mtakatifu huniambia hilo ni kosa. Ndipo ninatubu papo hapo, "Bwana, nisamehe. Sikukusudia kufanya hivyo. Unisaidie sasa." Nami ninaendelea moja kwa moja, jambo lile lile. Maana, mara tu inapotoka midomoni mwangu, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni wa haki ya kuzisamehe." Hiyo ni kweli? Haleluya!

136 Ibilisi anasema, "Unajua nini? Nitakwambia. Ulipaswa kwenda kufanya jambo fulani. Hukulifanya. Uh-huh, ulitenda dhambi, sivyo?"

Nasema, "Niliungama."

"Vema, nakwambia . . . "

137 "La, usizungumze nami. La, bwana. Nina imani kamilifu katika Yeye aliyeniambia nikiungama makosa yangu, angenisamehe. Kwa hiyo, ninaungama. Ondoka kwangu. Sijali chochote kukuhusu, kwa vyovyote vile, kwa hiyo endelea kusonga mbele tu."

138 Tembea kwa ujasiri, moja kwa moja uingie ndani yake. Kama mauti iko pale, hiyo ni sawa, endelea moja kwa moja uingie ndani yake, kwa imani kamilifu, kwamba, Mungu ameahidi kwamba "atawafufua katika siku za mwisho." Naam, bwana.

139 Kama nilivyokuwa nikiwaambia; sijui kama niliwaambia au la. Hapa siku chache zilizopita, kabla sijaenda ng'ambo, nilikuwa nimesimama, nami pamoja na Gene tulikuwa karibu kufanya kama ulivyosema. Nilikuwa nikijaribu kuchanua, zile, nywele zilizosalia. Mke wangu akaniangalia. Akasema, "Mpenzi! Hum!" Akasema, "Afadhali uvae moja ya vipande hivyo vya nywele walizokupa hapa California."

140 Nikasema, “Mpenzi, ninavipenda sana, lakini ninaona aibu tu kuvivaa.”

141 Akasema, “Jamani, Bill, hakika unachukua ninii zako... Nywele zako zimepotea kweli, sivyo?”

142 Nikasema, “Naam, hiyo ni kweli. Lakini,” Nikasema, “loo, haleluya!”

Akasema, “Unasema ‘haleluya’ ya nini?”

Nikasema, “Kamwe sikuwahi kupoteza hata moja ya hizo.”

Akasema, “Ati hujawahi kupoteza hata moja?”

143 Nikasema, “La.” Nikasema, “Unaona, mpenzi, ninazeeka.” Nikasema, “Nina umri wa miaka arobaini na mitano.” Nikasema, “Mimi ni mzee.” Kasema, “Mimi si...Jamani,” Nikasema, “Ninazeeka. Mimi...haileti tofauti yoyote kwangu kama nina upara ama nini. Haijalishi kwangu, maadamu siendi, si—sipati homa mbaya kwa urahisi sana. Naam.”

144 Naye akasema, “Vema...” nikasema...Lakini akasema, “Naam, ni wapi wewe...” Kasema, “Lakini ulisema nywele zako hazijapotea.”

145 Nikasema, “Hazijapotea. Mbona,” nikasema, “Yesu alisema, ‘Hakutakuwa na unywele mmoja wa kichwa chako utakaoangamia.’” Mnaona? Mnaona?

Akasema, “Unamaanisha...Vema?”

146 Nikasema, “Mpenzi, katika ufufuo, nitakapotokea, kuwa kijana mwanamume kama nilivyokuwa tulipooana; bega lililonyoka, hamna kunyanzi, nywele nyeusi zenye mawimbi.” Nikasema, “Hivyo ndivyo nitakavyoonekana tena.” Naam, bwana. Nikasema, “Kamwe sitapoteza mmoja wa hizo basi.”

Kasema, “Vema, vema, ziko wapi?”

147 Nikasema, “Nitakuuliza kitu fulani, halafu, ukinijibu, nitakujibu.”

Akasema, “Kitu gani?”

Nikasema, “Zilikuwa wapi kabla sijazipata?”

Akasema, “Naam, nadhani Mungu alikuwa...”

148 Nikasema, “Huko ndiko aliko nazo, pia.” Nikasema, “Bado zingali kule. Kila vitamini iliyokuwa ndani yake, kila seli ya uhai iliyokuwa ndani yake, kila atomi iliyokuwa ndani yake, kila sehemu ya petroli iliyokuwa ndani yake, kila sehemu ya nuru iliyohitajika kuzitengeneza, Mungu alikuwa nazo mikononi Mwake. Hakuna hata mmoja wa hizo ulioangamia. Ziko, kila moja yazo, mahali fulani mikononi mwa Mungu.”

149 Ninaangalia, macho yangu yanainama chini, mpwayo hapa chini, makunyanzi makubwa kwenye paji la uso wangu. Na wakati mwingine karibu inanibidi kufinya macho, kuiangalia Biblia yangu. Naye daktari aliniambia nilikuwa na macho

mazuri sana, ishirini kwa ishirini, lakini akasema, “Ukiisha kupita umri wa miaka arobaini, mboni zako za macho zinakuwa bapa, wala huwezi kusoma karibu sana nawe.”

Nilkasema, “Naam, bwana, najua hilo.”

150 Akasema, “Unaendelea kusukuma Biblia yako mbele, na Biblia mbele.” Kasema, “Baada ya muda kidogo, unaiweka *huku* mbali sana.”

151 Nikasema, “Nitachukua tu ya herufi kubwa zaidi, ama kitu kama hicho.”

Akasema, “Naam, ni mambo ya maumbile tu.”

152 “Ninaangalia *huko* nje, nami ninaweza kuona unywele mwishoni mwa sahani.”

153 Akasema, “Vema, una umri wa miaka arobaini, bwana.” Akasema, “Mboni za—za macho yako zinaninii tu. . .Kama vile tu nywele zako zinavyoingia mvi, na kadhalika,” kasema, “inakubidi tu kuwa nayo.”

Nikasema, “U-huh.” Huh!

154 Niliangalia haya yote. Nami nikaangalia bega langu, nami nimesimama huku mabega yameinama. Kidogo nilikuwa kijana na mwepesi. Ninanenepa sasa. Nina pauni arobaini zaidi, za uzani. Na nina nyayo bapa, kwanza kabisa, na sasa ni vigumu kutembea-tembea. Maumivu na uchungu unakuja. Vema, ninazeeka, hivyo tu.

155 Sihitaji madoido haya yote hapa niliyokuwa nayo, bali sijapoteza zozote. Kila mita iliyokuwa ndani yao, ngozi, iliyonifanya mchanga, Mungu bado anazo. Hiyo ni kweli.

156 Nalo ganda hili la kale, likienda tu kwa kujikokota, ni hivyo tu. Baada ya kitambo kidogo, litazeeka na kuingia makunyanzi, na labda kama vile akina Harvey wengine wanavyofanya, upande wa mama yangu. Ambapo, walisema ninafanana na Harvey. Wote hushikwa na ugonjwa wa kupooza. Nyote mnamkumbuka babu, yule aliyelijenga hili kanisa hapa, mwajua. Daima anatetemeka, anaenda namna *hiyo*, mnaona, na ana ugonjwa wa kupooza.

157 Nilimwona maskini mama mkongwe, hivi majuzi. Natumaini hayuko hapa, lakini . . . [Dada mmoja katika kusanyiko anasema, “Naam, yuko.”—Mh.] Loo, sijui kama . . . Vema, hata hivyo, alianza kunywa kikombe cha kahawa, na maskini huyo mkongwe namna *hiyo*, na mikono yake mizee namna hiyo. Nami nikaangalia makunyanzi yaliyoning’inia. Nikawaza, “Loo, rehema!” Afadhali niliseme. Ameketi pale, mnaona. Kasema, “Mimi si . . . ? . . . ” Naye anaweza kustahimili. Lakini, basi angalieni, moyo wangu karibu uruke kinywani mwangu. Nikageuza kichwa changu. Nikawazia, “Mungu, ni mara ngapi hayo yalitoa machozi machoni mwangu, na sasa ana ugonjwa wa

kupooza, anatetemeka!" Nikawazia, "Naam, nitafikia, pia, siku moja, mahali hapo, kama nikiishi."

158 Lakini, ndugu, moja ya siku hizi, nitaninii tu... Magurudumu ya kale ya maisha yanayopatikana na mauti yote yatasimama kimya. Yatakaposimama, nitaenda huko kwenye kilima cha Sayuni, kuishi kwa muda Huko. Naam, bwana. Mambo haya yote ya kibinadamu! Loo, kumbukeni, alisema:

> Kesho yenye furaha yaningojea,
> Ambapo malango ya lulu yatafunguliwa wazi,
> Na nivukapo pazia hili la huzuni,
> Nitapiga kambi Ng'ambo ya pili.
>
> Siku moja wasikofika viumbe wafao,
> Siku moja, Mungu anajua tu ni wapi na lini,
> Magurudumu ya maisha ya kibinadamu yatasimama kimya,
> Ndipo nitakwenda kukaa juu ya mlima Sayuni.
>
> Pembea chini, gari tamu,
> Linakuja kunipeleka Nyumbani;
> Pembea chini, gari tamu,
> Linakuja kunipeleka Nyumbani.

159 Hiyo ni kweli. Ukungu utaanza kutiririka mbele ya uso wangu, labda daktari ataingia mbio na kusema, "Vema, Billy, yote yamekwisha." Loo, jamani! Ninajua kile chumba cheusi cha kale kiko kule, na moyo unadunda, ukiingia moja kwa moja humo. Sitaki kwenda kama mwoga. Ninataka kujivika majoho ya haki Yake, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake. Na siku moja atakapoita, nitatoka miongoni mwa wafu, na kuishi tena milele.

160 Kumjua Kristo ni kujua Uzima. Hiyo ni kweli. Wala sijali, huenda nisijue ABC zangu, bali nataka kumjua Kristo. Hiyo ni kweli. Huenda nisijue theolojia yote, lakini nataka kumjua Kristo. Huenda nisijue kuhusu Rais, na kama yeye ni mtu mzuri au mbaya. Nataka kumjua Kristo. Hiyo ni kweli. Kumjua Kristo ni Uzima. Hiyo ni kweli. Kumjua Rais na kumjua huyu mwingine, ni fahari, na kuwajua watu mashuhuri na kadhalika. Lakini sijali kuhusu hayo. Ninataka kumjua Kristo katika Nguvu za kufufuka Kwake, nikijua kwamba tunaye, usiku wa leo, "Kuhani Mkuu anayeketi mkono wa kuume wa Mungu, katika ukuu Wake Kule, akifanya maombezi." Halafu, nataka kushika sana maungamo hayo!

161 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...- mbele ya dini kumi na tatu mbalimbali, za waabudu nyoka na waabudu ng'ombe, na kila kitu. Nikasema, "Waungwana, wa dini za ulimwengu huu, dini yenu inaweza kutoa nini kwa maskini kipofu huyu aliyesimama hapa?" Huyo hapo, aliliangalia jua kwa miaka ishirini. Alikuwa kipofu kabisa. Nikasema, "Dini yenu inaweza

kumfanyia nini mtu huyu?" Hakuna kitu ulimwenguni ila kumpa aina fulani ya kitu cha kubuni huko nje, kinachosema, "Labda siku moja, Muhammad amrehemu na kuiokoa nafsi yake." Labda, ndivyo mnavyowazia, "kama angali analiangalia jua, na kuendelea na kuendelea, na kukiweka kichwa chake hivyo, atakapokufa, ataokolewa."

162 Nikasema, "Hamwezi kutoa chochote. Lakini Damu ya Yesu Kristo, haleluya, si kwamba tu itampa Uzima wa Milele, bali ninaweza kulithibitisha papa hapa mbele zenu, inaweza kumrudishia macho hayo aliyokuwa nayo huko nyuma." Nikasema, "Ikiwa Yeye atafanya hivyo, je, enyi waungwana, wa dini za ulimwengu huu. . ." Wakati, karibu mamia ya maelfu ya watu walikuwa wakisikia jambo hilo, na walikuwa wamekusanyika mle. Bila shaka, nisingeweza kuwafikia wengi hivyo, wakasikie, maana usingeweza kuwaona wengi hivyo. Lakini nikasema, "Je, mtamkubali Yesu Kristo kama atafanya hivyo?" Wakainua mikono yao, hiyo mikono myeusi hewani, wangefanya hivyo. Nikasema, "Mlete huyo muungwana hapa."

163 Alipofika pale, nikasema, "Bwana, wewe ni kipofu. Na kama Yesu Kristo atakurudishia macho yako, je, utaahidi utamtumikia?"

164 Naye akasema, "Nitampenda Yesu Kristo, na nisiabudu Mungu mwingine ila Yeye. Kama atanirudishia macho yangu, nitajua ya kwamba alifufuka katika wafu."

165 Nikaweka mikono yangu juu yake. Nikasema, "Mungu mpendwa, kama mikono ipatikanayo na mauti, mtu mfanyi kazi, mtu mwenye dhambi; lakini kama unatafuta mikono mitakatifu, ni nani angekuwa nayo? Lakini ninakuja kwa tendo la imani, ambalo uliniambia nifanye. Na mimi naja, si kuwa mwerevu, ama kujisifu, bali ninakuja kwa sababu Wewe ulisema wanapaswa kufanya hivyo. Nami ninaamini Neno Lako. Na sasa wakati maelfu wakiwa hapa, wamesimama tu ukingoni, nao wanaabudu sanamu na chochote kile, na ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ndiwe Mungu wa kweli na aliye hai aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, kwa kumpa mtu huyu kuona kwake."

166 Ndipo yule mtu, huku machozi yakitiririka shavuni mwake, akasema, "Naona." Naye huyo akapitia humo jengoni, upesi alivyoweza kwenda, huku anaona. Loo, jamani!

> Hiyo ni neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, (Huko nje, mbio za farasi na chochote kile Jumapili.)
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

167 Angalia, ndugu, ni dini hii nzuri, ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu.

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
Neema ndiyo imeondoa hofu zangu;
Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
Saa niliyoamini kwanza! (Naam, bwana! Loo, jamani!)

Tukishakuwa huko miaka elfu kumi,
Tuking'aa sana kama jua;
Hatutakuwa na siku pungufu kuimba sifa Zake
Kuliko tulipoanza mara ya kwanza. (Loo, jamani!)

Kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,
Nimekuja tayari;
Neema ndiyo iliyonifundisha, au, ilinifikisha salama umbali huu,
Neema ndiyo itakayonipeleka mbele. (Loo, jamani!)

168 Jinsi ninavyompenda! Ni neema Yake, si chochote ningeweza kufanya. Hakuna nilichoweza kufanya. Hakuna unachoweza kufanya. Lakini, sisi, tukija usiku wa leo, kama Wakristo wanaume kwa wanawake, tukikiri kwamba hatustahili, na kumkubali kama wetu...badala yetu. Kumkubali Huyo ambaye...Najua, kwa hakika kama vile Mungu alivyomkubali na kumwinua, aliniinua katika mfano wa umbo, wakati ule ule alipomfufua Kristo. Amina. Loo, sina budi kusimama. Lakini, tazama. Katika mfano wa umbo, alinifufua wakati ule ule alipomfufua Kristo. Alikufufua wakati ule ule alipomfufua Kristo, kwa maana hiyo ilikuwa kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

169 Angalieni, kama umeokolewa, unayo. "Wale ambao amewakusudia, au kuwaita, amewahesabia haki. Wale ambao amewahesabia haki, tayari amewatukuza katika Kristo Yesu." Hiyo ni kweli? "Amewatukuza," tayari, "katika Kristo," kwa macho ya Mungu, Yule ambaye huko nyuma kabisa, mamilioni ya miaka kabla ya kuwepo kwa ulimwengu, wakati huyo Neno alipokuwa pamoja na Mungu. Lilikuwa ni wazo la Mungu, kisha Neno Lake, kisha likafanyika mwili huko ng'ambo. Na wakati ule ule alipomkubali Kristo, alinikubali katika Kristo. Na huko, katika ulimwengu ujao, mimi na wewe na Wakristo wote katika nyakati zote, tutampenda na kuishi pamoja Naye, na kufurahia Umilele usio na mwisho pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo, Mkombozi wetu aliyebarikiwa. Loo, jamani!

170 Ndugu Roberson, hilo linanifanya nijisikie kama mtu tofauti. Unaona? Je, mtindo wa kale, kusoma tu Neno la Mungu,

hakukusugui tu? Unaona, kunakusugua tu!

171 Kama mama alivyokuwa akifanya, wakati wa gudulia la matunda. Ilibidi kutia koponi magudulia ya matunda, mwajua, kuyajaza vihifadhi ubora na kadhalika. Angenifanya niende huko nje na kuyasugua, kwa nguvu tu niwezavyo kwa kitambaa cha kale. Nilikuwa na mkono mdogo, kuutumbukiza mle na kuyasugua. Halafu angeyachukua na kuyasafisha. Anayaweka kwenye maji moto, na kuyasafisha. Anayachemsha tu sana awezavyo, hayo magudulia. Singeweza kuona ni kwa nini aliyachemsha. Lakini alitaka kuondoa vijidudu vyote kwayo. Maana, kama kungekuwa na vijidudu mle ndani, vingefanya vile vihifadhi ubora, ama vile vitu alivyoweka humo, vichachuke.

172 Basi hivyo ndivyo tunavyohitaji kufanya tunapomjia Kristo. Tushuke kule mpaka Roho Mtakatifu ametusafisha na kutuchemsha kabisa, ndipo Mungu anaweza kumweka Roho Mtakatifu mle, pasipo na mchachuko wowote, mnaona. Yeye anamweka tu humo ndani, nawe ni mtamu tu wakati wote.

173 Naye mama alikuwa akipika vihifadhi ubora. Je, mliwahi kuona mojawapo ya hizo birika kubwa za kale? Unatoka nje na kuiweka juu ya matofali, unajua, na inakubidi kutia kuni chini yake namna hiyo. Uh! Nimewahi. Katika wakati uliowekwa wa kupika, alikuwa na maskini hizo nyanya ndogo manjano, za kibuyu. Naye angemwaga kama pishi moja yao mle, na kutia sukari. Uh! Na—naye angenituma kukata kuni, mwajua. Na—nami ningeenda kukata kuni na kuzitia chini pale, mwajua, nayo ya—yangeanza kuchemka. Mvuke ungetokea. Nikasema, “Mama, kwani vitu hivi havijaiva?”

Akasema, “La. Nenda ukakate kuni zingine uani.”

174 Mimi huyu hapa naja, mwajua, huku natokwa na jasho, na kuziweka pale chini. Ndipo ningesema, “Mama, unafikiri hizo zitatosha?”

“Afadhali ukalete zingine.”

175 Naye angevifanya vitu hivyo vichemke mpaka vingeninii, mwajua, o—oksijeni au kitu fulani kingeingia chini yake, na kuyafanya yatokote, mwajua, “po, po,” namna hiyo, kutokota. Yalipokuwa hivyo, alisema yalikuwa tayari kutiwa koponi. Yalipata joto sana, hayangeweza kustahimili tena, ikabidi yaruke, mnaona.

176 Kwa hivyo nadhani hivyo ndivyo tu Mungu hana budi kutukuta, mwajua, amchemshe tu ibilisi wote akuondokee mpaka unaruka katika utukufu. Ndipo uko tayari kutiwa koponi. Naye Mungu akakutia muhuri basi, unajua. Kwa hiyo hilo ndilo tunalohitaji hapa, ni mkutano mzuri wa mtindo wa kale, hata uadui wo—wote, kila kitu ambacho hakifanani na Kristo, kichemshwe kabisa kitoke, mnaona. Uchemshwe tu mpaka uje tu, “Bwana, samahani.” “Ndugu, nisamehe. Sikukusudia kufanya hivyo. Si—sitafanya hivyo tena.” “Ee

Mungu, unirehemu!" Hapo, unakuwa tayari kutiwa koponi basi, unaona. Mungu anajiandaa kukutumia kweli. Unaporudisha vitu hivyo, ulivyoiba, wajua, na kurekebisha hilo, ukisema, "Ndugu, sikukusudia kuiba hivyo, wajua. La, bwana. Ni—niko tayari hata...ni—nitakulipa hizo maradufu." Unaona? Basi unakuwa sawa, basi, wajua. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo tunalohitaji. Loo, jamani!

177 Nitawaimbia *Dini ya Zamani za Kale* mkitaka niwaimbie. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Imbeni aya, nitaimba aya. Mnaimba pambio, basi.

Ni Roho Mtakatifu wa zamani za kale,
Wala ibilisi hataikaribia,
Hiyo ndiyo sababu watu wanaiogopa;
Bali ni nzuri vya kutosha kwangu.

Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Itafaa ninapokufa;
Itakufanya uache udanganyifu wako;
Itamfanya ibilisi atoroke,
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Na ni nzuri vya kutosha kwangu. (Mnaona?)

Ni nzuri sana sitaki nyingine,
Kwa kuwa inanifanya kumpenda ndugu yangu;
Nayo inatoa mambo yaliyofichika,
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nipe hiyo dini ya zamani za kale,
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

178 Sasa, ni wangapi hapa walio na hiyo dini ya zamani za kale? Inua mkono wako, useme:

Ninayo hiyo dini ya zamani za kale,
Ninayo dini hiyo ya zamani za kale,
Ninayo dini hiyo ya zamani za kale,
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

179 Sasa, Baba Mpendwa, sisi wakati mwingine...Nasi hufurahi na kufanya kama kundi la watoto. Hiyo ni kwa sababu tuko huru. Hatuko chini ya utumwa wa uovu, au mapokeo yoyote, au mambo fulani ya wazee. Tuko huru tu katika Roho Mtakatifu, hata tunaweza kuimba na kukuabudu, na kushiriki kwenye Neno, na kujifurahisha. Kwa hilo, tunakusifu Wewe,

Mwenyezi Mungu! Loo, baada ya kuona machafuko yote ya dini baridi, na kila aina ya ibada za sanamu; na kuwazia kwamba ulikuwa mwema sana, kwangu, kunijalia nikujue Wewe katika Nguvu za kufufuka Kwako, na kuweza kuwaambia wengine juu yake. Tuna furaha sana.

180 Libariki kanisa hili dogo, usiku wa leo, Baba. Mbariki kila mtu hapa. Ikiwa kuna wageni malangoni petu, wabariki, Baba, kila mmoja. Utufanye kuwa baraka kwa wengine. Weka Nguvu za Mungu juu yetu. Takasa nafsi zetu kutokana na mawazo mabaya. Na kama uovu utatujia, jalia tugeuze vichwa vyetu upesi, Bwana, na tupitie hiyo njia nyingine.

181 Na sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utatubariki pamoja, usiku wa leo. Tupe wakati mzuri. Na sasa, tutakapowaita wagonjwa na wanaoteseka, tunaomba ya kwamba utaponya kila mmoja wao. Jalia utukufu. . .Pata utukufu kutoka kwa yote yaliyofanywa au kusemwa, kwa maana tunaomba katika Jina la Kristo.

182 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, kama yeyote wenu hapa, angesema, "Ndugu Bill, nafsini mwangu tu sasa, ni—ningependa kuja tu kwa njia ya Mungu iliyokubalika, na njia iliyoandaliwa. Na ningependa kuwauliza, wakati hakuna mtu mwingine anayeangalia, nitainua mkono wangu na kusema, 'Ndugu Bill, niombee, kwamba Mungu atanipa tu neema Yake na kunifanya Mkristo bora zaidi.'" Je, unaweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Hilo ni zuri. Vema.

183 Baba, unaiona mikono yao, nami naomba ya kwamba utatujalia baraka hizi. Upendo Wako na neema ziwe juu yao wote. Na kama wametenda dhambi, ama wamefanya jambo lolote, basi, Baba, ninaomba ya kwamba uwasamehe. Kama kuna yeyote miongoni mwetu, usiku wa leo, Bwana, popote pale jengoni, mwanamume au mwanamke, mvulana au msichana, ambaye hajaokoka tu hasa, na yuko chini ya Damu, Baba, ninaomba ya kwamba utafanya hivyo sasa hivi, na jalia wawe waaminio.

184 Nawe umesema, "Kama unaweza kuamini." Na tunaamini nini? Tunaamini kwamba Mungu alimtuma Mwanawe katika ulimwengu huu, naye akafanywa kuwa dhambi, badala yetu. Na sisi si wema, na tunakiri kwamba sisi si wema hata kidogo; na kumkubali kama Mwokozi wetu. Hilo ndilo tunaloamini, Baba. Katika hilo, unatupa Uzima wa milele. Loo, tuna furaha sana! Ulisema utatupa kwa sababu tulikuwa tumemwamini Mwanao. Naye Yesu alisema, Mwenyewe, ya kwamba kama tulimwamini, ya kwamba tulikuwa na uzima wa milele. Kwa hiyo, tunashukuru kwa jambo hili.

185 Sasa, tubariki, usiku wa leo, na usamehe kila dhambi. Na jalia kusiwe na mtu hata mmoja, ambaye amekuwa katika mkutano huu usiku wa leo, atakayewahi kufukuzwa, bali na

wapate uzima wa milele, kwa sababu wamekusanyika hapa usiku wa leo na wamekuamini Wewe. Na, Baba, ninaomba ya kwamba utawaangalia sasa, na kuwabariki katika yote wanayofanya ama kusema. Na jalia waje Kwako kwa amani, katika siku za mwisho. Jalia sisi sote tukusanyike Huko, na tukumbuke usiku huu, tukiwa pamoja. Tujalie, kwa Jina la Yesu. Amina.

186 Mungu awabariki, rafiki zangu wapendwa. Na sasa Teddy atakuja hapa kwenye piano. Na wale wanaopaswa kuombewa, kama mtakusanyika kuzunguka madhabahu, upesi sana. Tutakuwa tu na dakika chache zaidi. Tutajaribu kutoka nje saa tatu na nusu, ikiwa mtakuja sasa. Vema, nina barua hapa ya kusoma, kuna mtu fulani amenituma hapa. Huenda ikawa muhimu kwangu kuisoma sasa hivi. Kwa hiyo ninii tu . . . Nanyi wengine bakini vitini mwenu, huku wale wa kuombewa. Najua Dada Ruddell yuko hapa kuombewa. Endapo mtu mwingine yeyote, mbona . . .

54-1006 Torati Ama Neema
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org